HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI MHE. MHANDISI EVARIST W. NDIKILO WAKATI WA KIKAO CHA WADAU WA SEKTA YA MAJI VIJIJINI MKOA WA PWANI TAREHE 05 FEBRUARI, 2021 KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA

Mhe. Mwenyekiti wa CCM Mkoa,

Ndg. Katibu Tawala wa Mkoa,

Wahe. Wakuu wa Wilaya,

Ndg. Katibu wa CCM Mkoa,

Wahe. Wabunge,

Wahe. Wakuu wa Wilaya,

Ndg. Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa,

Wahe; Wenyeviti wa Halmashauri,

Ndg. Meneja RUWASA Mkoa,

Ndg.Wakuu wa Idara na Vitengo Sekretarieti ya Mkoa,

Ndg. Wakurugenzi wa Halmashauri,

Ndg. Wajumbe wa Kamati ya Amani ya Mkoa,

Ndg. Ma - Meneja wa RUWASA Wilaya,

Ndg Sekretarieti ya Kikao,

Ndg. Wanahabari na Wageni waalikwa,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo kwenye Mkutano wa Kwanza wa Wadau wa Sekta ya Maji Vijijini, ikiwa ni mara yetu ya kwanza kukutana. Tumeanza kukutana sisi Viongozi na Wawakilishi wa Wananchi, na nimeambiwa Wakala (RUWASA) siku zijazo wataendelea kukutana na watumiaji ambao ni wananchi wenyewe.

Pili, nimpongeze Katibu Tawala wa Mkoa na Meneja wa RUWASA Mkoa kwa kuandaa Mkutano na kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika Mkutano huu.

Tatu, ninawashukuru wajumbe wote mlioalikwa na kufika kushiriki Mkutano huu. Lakini pia kwa wale ambao hawakufika kwa sababu mbalimbali naamini watapata fursa ya kushiriki nasi vikao vijavyo.

Ndugu Wajumbe,

Ikiwa ni mara ya Kwanza kufanyika kwa Mkutano huu nimefarijika na ushiriki wa wabunge ambao wapo majimboni, Wenyeviti wa Halmashauri, ni matumaini yangu kuwa utakuwa ni Mkutano wenye tija utakaoweka mipango ya kutatua kero za Wananchi. Na kumsaidia Mhe Rais kufikia malengo yake ambayo yapo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Niseme RUWASA Mkoa wa Pwani mmeanza Vizuri, tuendele kwa ushirikiano huu**, Hongereni sana.**

Ndugu Wajumbe,

Tumekutana leo hii kubwa likiwa kushirikishwa Mipango ya Wakala huyu wa Maji Vijiijini (RUWASA) ili na sisi Viongozi tutoe mapendekezo na Ushauri wa namna ya kuboresha upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini kwenye Maeneo yetu yaliyofikiwa na huduma hii lakini na kufikisha katika maeneo ambayo haijafika kabisa.

Hivyo, niwaombe nyote kushiriki Mkutano huu kikamilifu kwa kutoa maoni na mapendekezo ili kuwasaidia RUWASA kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya Maji Vijijini.

Ndugu Wajumbe,

Mkoa wetu wa Pwani unakuwa kwa kasi Kiuchumi na Kijamii, idadi ya watu inaongezeka kila siku. Uhitaji wa huduma za Kijamii kama vile Maji, Afya, Elimu nao unaongezeka. Aidha, uhitaji wa Miundombinu ya Kiuchumi kama vile Umeme, Barabara, Usafirishaji, Masoko, Stendi, Maghala n.k pia umeongezeka.

Pamoja na kuongezeka kwa Mahitaji ya huduma hizo za Kijamii ni dhahiri kabisa kuwa Miundombinu ya Kichumi pia inatakiwa kwenda sambamba na ukuaji huo, jambo ambalo Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dkt John Pombe Magufuli imefanya kazi kubwa ili kukidhi haja ya mahitaji ya huduma hizi za kijamii na Kiuchumi.

Miradi mikubwa ya Kijamii Mkoa wa Pwani iliyotekelezwa katika kipindi cha kwanza (2015-2020) cha Mhe. Rais akiwa madarakani na yenye lengo la kuleta maendeleo ya haraka kwa Mwananchi na kusaidia kuinua hali ya kiuchumi na Kupunguza umasikini ni pamoja na:-

i. Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya afya 18 (**Sh.8.2 bn/-)**

ii. Ujenzi wa Hospitali tatu **(Sh.4.5 bn/-)**

iii. Ujenzi wa Zahanati

iv. Elimu bila malipo

v. Ukarabati wa shule kongwe,

vi. Miradi ya maji kisarawe (**Sh. 10 bn)**

vii. Mradi wa maji Mlandizi - Chalinze - Kijiji cha Mboga kwa

(Sh 17.7 bn)

viii. Mradi wa Maji Mkuranga tanki lita 1.5 (**sh. 5.6 bn**)

ix. Ujenzi wa Kivuko kipya cha Kibiti Nyamisati **(sh. 5.3 bn)** na mingine mingi.

Na hivi sasa Serikali inakamilisha taratibu za kuendeleza mradi wa upanuzi na uboreshaji wa Hospitali ya Mkoa ya Tumbi ili iwe na miundombmu inayokidhi hadhi ya kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. **Hongera Rais wetu**

Ndugu Wajumbe,

Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 Ibara 100 imelenga katika kipindi cha miaka mitano ijayo kufikia 2025 huduma ya Maji safi na salama kuwafikia zaidi ya 85% ya wakazi wa vijijini na zaidi ya 95% ya wakazi wa Mijini**.**

Hadi kufikia mwezi Januari, 2021 wastani wa 73% ya wakazi wote wa Mkoa wanapata huduma ya maji safi na salama ikiwa asilimia **71%** ya wakazi waishio Vijijini wanaopata huduma ya maji na 84 % ya wananchi waishio mijini wanapata huduma hiyo katika Mkoa wa Pwani.

Ndugu Wajumbe,

Kwa mkazo huo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020, Mhe Rais Dkt John POMBE Magufuli wakati wa hotuba yake ya kufungua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma tarehe 13 Novemba 2020, Mhe Rais alisema ***"nilipokuwa kwenye Kampeni changamoto kubwa aliyoelezwa na Wananchi ilikuwa ni shida ya Maji hususani maeneo ya Vijijini.***" Mhe Rais ameelekeza Nguvu kubwa kwenye miaka hii mitano ijayo kuhakikisha anatatua changamoto ya ya Maji kwenye maeneo yetu. Hivyo hatuna budi sisi wasaidizi wake wote

kuhakikisha maono ya Mhe Rais na maelengo yake ya kuondoa shida ya maji yanafikiwa. Na ndiyo maana tumekutana hapa leo.

Ndugu Wajumbe,

Hata hivyo Katika Kipindi cha Uongozi wa Awamu ya Tano huduma ya Maji imeboreka kwenye Mkoa wetu ukilinganisha na miaka ya nyuma, Ipo miradi iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa maeneo mbalimbali ya Mkoa wetu. Miradi hii inatekelezwa na Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini RUWASA, sambamba na ile inayotekelezwa na DAWASA.

Kwa upande wa Maji Vijijini Nimeambiwa Miradi 26 yenye thamani ya Shilingi 3,930,685332.36 mipya (5) na ambayo imefanyiwa ukarabati (21) imekamilika chini ya Usimamizi wa RUWASA ndani ya Kipindi cha miaka miwili mwaka 2019 hadi sasa. Miradi hiyo imenufaisha wakazi 38,889. **Hongereni RUWASA kwa kazi nzuri.**

Miradi hiyo mipya (5) iliyokamilika ni pamoja na:-

- Mradi wa maji Jibondo (Mafia),
- Mradi wa maji Yavayava (Mkuranga),
- Mradi wa maji Mianzi (Kisarawe),
- Mradi wa maji Yombo (Bagamoyo) na
- Upanuzi wa Mradi wa maji Ikwiriri (Rufiji).

Ndugu wajumbe,

Katika Kipindi cha kuanzia Julai, 2019 RUWASA imeendelea kutekeleza jumla ya miradi 48 yenye Gharama ya Shs. 9,829,086,448.77 ambapo itanufaisha wakazi zaidi ya 99,334.

Kati ya miradi hiyo 48 mipya ni (16) nayo inatekelezwa katika Halmashauri za:- Wilaya za **Chalinze (1), Bagamoyo (2), Mkuranga (4), Kisarawe (2), Kibaha (2), Kibiti (3), Rufiji (2),** kwa Gharama ya **Shs 8,403,232,539.94** itakayonufaisha jumla ya **Wananchi 77,760.**

Miradi inayofanyiwa ukarabati ni (32) ambapo ipo katika Halmashauri za Wilaya za **Chalinze (3)**, **Bagamoyo (5), Mkuranga (3**), **Kisarawe (1), Kibaha (3), Kibiti (3), Rufiji (8), Mafia (6)** Gharama ya Shs **1,425,853,908.83** itakayohudumia wananchi 21,574.

Ndugu Wajumbe,

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kutatua changamoto ya Maji hasa Vijijini tunatarajia kuletwa kwa fedha nyingi za Ujenzi na Ukatabati wa Miradi. Sisi Viongozi, Wawakilishi wa Wananchi, Watendaji wote wa Serikali kwa kushirikiana na wananchi ni wajibu wetu sasa:-

i. kuhakikisha miradi hii inatekelezwa kwa ubora,

ii. inaakisi thamani ya fedha (Value for Money)

iii. inakamilika kwa wakati.

iv. Aidha, tuhamasishe watumiaji ambao ni wananchi wetu kulinda vyanzo vya maji na miundombinu ya miradi hiyo ili miradi hiyo ili iwe endelevu.

Ndugu Wajumbe

Suala la ulinzi wa vyanzo vya maji ni letu sote. Sio suala la DAWASA au RUWASA ambao ni wazalishaji na wasambazaji wa maji na wala sio la Serikali. Ni suala ambalo kwa pamoja tunapaswa kulielewa na kuliishi kwa vitendo.

Mto Ruvu una faida nyingi kwetu. Tunapata samaki aina mbalimbali wakiwemo kambale na vitoga; tunautumia kusafiria kutoka eneo moja kwenda jingine kwa mitumbwi na tunatumia maji yake kwa shughuli mbalimbali za nyumbani na umwagiliaji. Njia pekee ya kuuwezesha mto huu kuwepo ili tuendelee kufaidi matumizi yake ni kutunza mazingira yake na hasa uoto wa asili.

Madhara ya kuharibu mazingira ni mengi. Kwanza ambayo nadhani kila mtu anajua ni kupungua kwa mvua na hatimaye kuwepo kwa hali ya ukame ambayo hupelekea mito na vyanzo vingine vya maji kama vile chemchemu na visima kukauka. Mazingira haya tunayaharibu kwa kukata miti, kuharibu uoto wa asili kwa kulima karibu na vyanzo na kulisha mifugo kwenye vyanzo.

Ndugu Wajumbe,

Madhara mengine ambayo ni lazima watumishi tuliopewa dhamana tusimamie kwa weledi, nguvu zetu zote na kwa kufuata sheria ni mapambano dhidi ya utupaji wa taka ngumu katika maeneo ya vyanzo vya maji na kuruhusu utiririshwaji wa majitaka yatokayo viwandani ambayo hayajatibiwa na kukidhi viwango katika mazingira yetu. Tusiposimamia utaratibu huu, tunaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa mazingira yetu na mwisho wa siku tukatumia gharama kubwa na muda mrefu kurekebisha makosa yetu.

Ndugu Wajumbe,

Pamoja na kuwa tumetangaza Mkoa wa Pwani kuwa Mkoa wa Viwanda; lakini ni lazima tuhakikishe kuwa viwanda tulivyonavyo vinakidhi viwango na sheria za mazingira na havileti athari katika mazingira yetu na hasa katika vyanzo vya maji.

Tukumbuke kuwa viwanda pia vinahitaji maji hivyo kama maji ya kutosha hayatazalishwa kutokana na upungufu wa maji unaotokana na kuharibiwa kwa mazingira; basi hata viwanda vitaathirika. Sote tukumbuke kuwa bila Mazingira kuwa salama na bila Maji hakuna Uhai.

Ndugu Wajumbe,

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na RUWASA, bado wanakabiliwa na changamoto kadha wa kadha. Miongoni mwa changamoto hizi ni pamoja na ukosefu wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi. Nitoe rai kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kutenga maeneo na kuwakabidhi RUWASA Kwa ajili ya Ofisi.

Mamlaka za Maji zilizochini ya RUWASA zinadai fedha nyingi kutoka Taasisi za Serikali, niombe Kupitia kikao hiki tuone umuhimu wa Taasisi zinazodaiwa kulipa ankara za maji ili Mamlaka hizi zijiendeshe kikamilifu.

Changamoto nyingine ni Ankara kubwa za maji inazotozwa Wananchi kwa Miradi ya Vijijini ambayo inatumia chanzo cha maji ya mabomba ya DAWASA. Mfano Mradi wa maji Ruvu Dosa hili jambo pia lifanyiwe kazi ili kuondoa changamoto hii (DAWASA Mkoa na RUWASA kutatua kero hii).

Niwakaribishe tena kwenye Mkutano wetu kwa lengo la kuuletea Mkoa wetu maendeleo.

Baada ya kusema hayo natamka kwamba mkutano wa siku moja wa wadau wa Sekta ya Maji vijiijini Mkoa wa Pwani umefunguliwa Rasmi.

AKSANTENI KWA KUNISIKILIZA.